KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na James L. Black, Sr. - Mratibu Huduma za Maombi: NAD

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

JUMA LA PILI: APRILI 10 – APRILI 16, 2020

MUUJIZA USIOTARAJIWA

Je! Umewahi kuona kitu kama hiki?" Hili ni swali la kawaida wakati watu wanaposhuhudia kitu fulani ambacho hawakuwahi kukiona kabla. Hakuna shaka jina "COVID-19" litaandikwa katika historia kama moja ya majanga makuu ya ulimwengu.

Ni jambo la ajabu namna maisha yanavyoweza kubadilika kwa haraka. Neno la Mungu linatukumbusha kwamba maafa yatakuja, na kuwa inatupasa daima kujiandaa na kumtegemea Bwana. Zahama hii ya ulimwengu imepasua kiini cha uchumi; mifumo ya afya imezidiwa; wengi wameachwa katika umasikini mkubwa; wengi wameachwa bila makazi na bila kazi; wengi wameachwa na maradhi ya kudumu; na ndiyo, zahama hii imeondoa uhai wa makumi elfu ya watu.

Wengi wanaomba kwa ajili ya muujiza. Wengi wanamsihi Mungu abadilishe hali zao na kuwalinda dhidi ya kirusi hiki cha kufisha. Lakini swali ni, Je! Tumejiandaa kwa ajili ya aina ya miujiza ambayo Mungu huitenda?

Sina mashaka kwamba Mungu atasikia na kuingilia kati kwa kila mmoja anayemwomba. Anapoingilia kati kwa njia tofauti na kwa wakati wake, ahadi hizi zinanipatia tumaini. "Hapatakuwa mtu ye yote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha" (Yoshua 1:5), na "Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa katika kunena, nitasikia (Isaya 65:24)"

Miaka kadhaa iliyopita nilipata ugonjwa wa mifupa uitwao kitaalamu MDS, yaani kudhoofika kwa chembechembe nyekundu za damu. Ikiwa ugonjwa huu ukiachwa bila kutibiwa hupelekea mtu kupata saratani ya damu au kifo. Nilikuwa katika hatua ya 4 ya ugonjwa huo, na tumaini langu pekee lilikuwa ni kufanyiwa upasuaji wa kupandikiza uboho (maji maji ya ndani ya mfupa). Maelfu ya watu ulimwenguni kote walikuwa wananiombea kwa ajili ya uponyaji nilipokuwa dhaifu kiasi cha kushindwa kuomba mwenyewe. Ndiyo, ninaweza kushuhudia kwamba Mungu aliingilia kati, lakini sio kwa njia iliyotarajiwa, kwani miujiza ya Mungu inahusu uzima wa milele.

Mambo matatu yalitokea yaliyomdhihirisha Bwana kwangu kwa njia ambazo sikuwahi kuzipitia kabla ya hapo. Jambo la kwanza, kwa sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo wangu kumudu, mchakato wa upandikizaji ulichelewa kwa miezi tisa ingawa nilikuwa katika hatua ya 4 ya ugonjwa. Huo ucheleweshwaji ulikuwa fursa kwa ajili ya matibabu ya kina ya ujumla na ya asili ambayo yaliuimarisha mwili wangu na kuuandaa kwa ajili ya upandikizaji. Jambo la pili, binti yangu, (aliyenipatia chembechembe za upandikizaji) na mimi tulipata muda wa kuungana na kuwa kitu kimoja kabla ya upasuaji, jambo hilo lilitupelekea kuwa na wakati wa kusameheana. Jambo la tatu ni kile kilichofanyika kwangu kwa ajili yangu na mke wangu. Kwa mara ya kwanza katika ndoa yetu, nilikuwa nimelalia mgongo wangu hospitalini, nikiwa na ugonjwa unaotishia maisha, nikiwa nimetengwa, nikiwa na uchovu sugu. Nilikuwa dhaifu kiasi cha

kushindwa kuoga, kwa hiyo, kama mara tatu au nne hivi, mke wangu Maxine ilimpasa kuniogesha. Mwanzoni nilikuwa nimekasirika, lakini nilipoona upole wake na kujitoa kwake kikamilifu alipokuwa akiniogesha tangu kichwani hadi kidole gumba, nilitambua kuwa Mungu alikuwa ananiandaa kwa ajili ya muujiza maalumu wa uponyaji.

Muujiza wangu wa pekee unapatikana kwenye maneno haya ya Yesu: "Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako (Marko 2:5)". Ndiyo, muujiza nilioupata nikiwa kwenye wakati wa uhitaji mkubwa ni kwamba Mungu aliniponya kabla ya upandikizaji. Kwa neema ya Mungu nilitoka hospitalini nikiwa kiumbe kipya ndani ya Yesu nikiwa nimeponywa magonjwa ya kiroho na kimwili.

Leo, ninakutia moyo uondoe macho yako toka kwenye COVID-19 na cho chote kinachokuvuruga, na kama wale marafiki wanne waliomleta aliyepooza kwa Yesu, toboa dari, njoo mbele za Yesu na umruhusu aiponye roho yako.

"Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa katika kunena, nitasikia" (Isaya 65:24)

Maswali ya Moyoni

Ingawa tunajua kwamba ni mapenzi ya Mungu kuwaponya watoto wake, kila mara hatujui mapenzi yake kuhuhu muda wa uponyaji. Wengine anaweza kuamua kuwaponya kwa haraka, wengine pole pole, wakati wengine anaweza asiwaponye hadi atakapokuja mara ya pili (Yakobo 5). Je! Tunaweza kumwamini Mungu na nyakati zake? Je! Tunaweza kusubiri kwa imani hata pale ambapo kila mara hatuoni majibu ya haraka kwa kwa maombi yetu? Tunawezaje kukuza imani yetu na kumtumainia Mungu na Neno lake?

Changamoto Hai ya Moyoni

Juma hili tunapoendelea kuombea wagonjwa, wataalamu wa afya, na kwa Mungu ili akomeshe kuenea kwa coronavirus ulimwenguni kote, hebu tuombe kwamba upendo kwa Mungu na Neno lake vienee. Hebu tuzifungue biblia zetu kwa shauku na kuomba, "Bwana, tuoneshe jinsi ya kukujua na kukupenda! Tuoneshe namna ya kupata uponyaji wa kweli kutoka ndani hadi nje. Tuoneshe maana ya kujifunza na kulielewa Neno lako. Na utuoneshe namna ya kushiriki na wengine Neno lako." Tunapoomba hebu tuzidai ahadi za Isaya 55:8-11, 2 Tim.2:15, na 1 Petro 3:15.

"Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako. Kwa moyo wangu wote nimekutafuta, Usiniache nipotee mbali na maagizo yako. Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi" (zab. 119:9-11)

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili

- Ellen White, *The Great Controversy, "Scriptures as a Safeguard,"* chapter 37
- Frank M. Hasel/Michael G. Hasel, *How to Interpret Scripture,* Companion book to Adult Sabbath School Study Guide for 2nd Quarter.

SIKU YA 15 - Aprili 10, 2020

Taarifa ya Sifa!: Inaonesha kwamba kuenea kwa janga kumeanza kupungua katika nchi ya Hispania na Italia. Tunamsifu Mungu kwamba kuna tumaini la mwelekeo mzuri.

MAMBO YA KUOMBEA

1. Tuombe kwamba Mungu azuie kuenea kwa COVID-19 kwenye nchi za ulimwengu zenye idadi kubwa ya watu. Kwa namna ya pekee tuombe Bwana aingilie kati India, Bangladeshi, bara la Afrika na baadhi ya nchi za Asia ambazo ndio zinaanza kupambana na janga la COVID-19 kwa nguvu zote.

2. Ombea watafiti wa madawa wagundue matibabu yanayoponya coronavirus maana hatuwezi kusubiri hadi miezi ya kutengenezwa kwa chanjo.

3. Tuombe Mungu awalinde watoto, watu dhaifu, na walio hatarini, wanaolazimika kukaa nyumbani na wanafamilia wenye kunyanyapaa na wanaoishi kwenye nyumba zenye hali ngumu.

4. Tuombe Mungu juu ya upatikanaji wa chakula na milo kwa watoto ambao hawaendi shuleni ambako walikuwa wanapata chakula kila siku.

5. Tuombe kwamba tuweze kujifunza Neno la Mungu kwa kina zaidi na pia kushiriki Neno lake kwa vitendo na wale wanaotuzunguka.

SIKU YA 16 - Aprili 11, 2020

TUFUNDISHE KUOMBA

“Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua” Yeremia 33:3

“Tumefikia nyakati makini. Matukio katika ulimwengu wetu yanamtaka kila mfuasi wa Kristo kuwa na jitihada kamili katika uhusiano wetu na Mungu. Kuimarisha uhusiano huu na kukidhi mahitaji yetu ya kihisia na kiroho, inatupasa kujifunza nguvu ya maombi, Ni lazima tumwombe Bwana, kama walivyomwomba wanafunzi wa kale, wakisema, ‘Bwana, tufundishe kuomba.” (Prayer, p. 1)

Maswali ya moyoni

Tunaweza kuwa tunashiriki Siku 100 za Maombi, na inawezekana tunaomba pamoja kwenye vikundi vidogo vya maombi, lakini Je! Tumejifunza kwa uhakika maana ya kuomba? Je! Tumewahi kulia kwa dhati kama wanafunzi walivyolia kwa Yesu wakisema, “Bwana, tufundishe kuomba?” Kama hujafanya hivyo, kwa nini usimwombe Bwana leo, “Tafadhali nifundishe kuomba!”

Taarifa ya Sifa

Ingawa mikutano iliyokuwa ifanyike kwenye jiji la Indianapolis ililazimika kuahirishwa, sasa, John Bradshaw anapanga kufanya mfululizo wa mikutano kwa njia ya mtandao ambayo tunaamini kuwa itaweza kuwafikia watu wengi. Tunatarajia makumi elfu ya watu watahudhuria. Kwa mara nyingine tena, lile adui alilokusudia kwa ubaya, Mungu analibadilisha kwa wema.

MAMBO YA KUOMBEA

1. Tuombe Mumgu atupe Roho Mtakatifu atufundishe jinsi ya kuomba kwa namna ambayo tutapokea majibu.
2. Tuombee mikutano ya injili kwa njia ya mtandao ambayo John Bradshaw na *It is Written* wanaipanga. Tuombe kwamba watu wengi waweze kuipata na kuyatoa maisha yao kwa Yesu.
3. Tuwaombee wataalamu wa afya na hospitali za maeneo mahalia zinazopambana na uhaba ya vifaa tiba. Tuombe Mungu atuwezeshe vifaa vinavyohitajika ili wataalamu wetu wa afya wawe salama.
4. Tuombe kwamba wawepo watengezaji wengi wa vifaa vya kujikinga, vitanda, vipunga hewa na majengo yawepo kwa ajili ya mahitaji ya huduma za afya
5. Tuombee Huduma kwa Wachina katika Jiji la Cebu., kule Ufilipino. Tuombee ulinzi dhidi ya coronavirus kwa kanisa na kwamba Wachina wengi wavutiwe kujifunza Maandiko

SIKU YA 17 - Aprili 12, 2020

USHINDI MKUU

Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza. (Zab. 50:15)

“Ushindi mkubwa unaopatikana katika kazi ya Mungu sio matokeo ya hoja zilizofanyiwa kazi, uwepo wa majengo, mvuto mkubwa, au uwingi wa mali; unapatikana katika chumba cha mazungumzo na Mungu, wakati watu wanapoushika mkono wa uweza wa Mungu wenye nguvu kwa bidii na imani yenye mateso. (GW 259).

Maswali ya Moyoni

Kwa vile tunajua kuwa tunapata ushindi wetu mkuu kwa njia ya maombi na kuwa na muda katika Neno la Mungu, kwa nini tunasita-sita kutenga muda wa kuomba na kujifunza Biblia? Ni shughuli au mambo gani yanayotuvuruga tusiwe na mawasiliano binafsi na Mungu?

Taarifa ya Sifa

Katika mji wa Qeensland kule Toowoomba (wenye watu 130,000), kuna makanisa mawili, Toowoomba Central na Glenvale . Mchungaji Casey Wolverton anachunga kanisa la Glenvale. COVID-19 ilipoingia na makanisa kufungwa, katika S abato ya kwanza, waliendesha huduma kama kawaida, lakini hakukuwa na mtu kwenye viti na ilirushwa kupitia mitandao ya Facebook na Yutube na watu 900 walitazama huduma hiyo. Kituo cha redio mahalia kilisikia kile Waadventista walichokuwa wakifanya, na wakawaendea Waadventista ili waweze kurekodi ibada na kuirusha jumapili iliyofuata kwa wasikilizaji 130,000. Kama kusingekuwa na COVID-19 uwezekano ni mdogo kwamba jambo hilo lingetokea. Tumsifu Mungu.

MAMBO YA KUOMBEA

1. Tuombe kwamba ujumbe maalumu wa matumaini uendelee kurushwa katika mji wa Toowoomba kule Qeensland, Australia. Tuwaombee washiriki wa kanisa kule Australia, ili watafute njia za kuendelea kuwa nuru kwa watu wanaowazunguka.
2. Tuwaombee Wainjilisti wetu wa vitabu kote ulimwenguni ambao hawawezi tena kuingia nyumba kwa nyumba. Tuombe Mungu afungue njia mpya kwa watendakazi waliojiweka wakfu kushiriki ukweli na wengine. Tuombe Mungu awapatie mahitaji yao.
3. Tuziombee hospitali katika nchi ya Marekani zinazotarajia kuwa na juma lingine gumu zaidi katika kushughulika na janga la COVID-19. Tuombe Mungu aingilie kati.
4. Tuwaombee wazee, wenye kinga dhaifu za mwili, na washiriki wengine walio katika hatari kubwa katika kanisa lako mahalia. Omba kwamba mkono wa ulinzi wa Mungu uwazunguke.
5. Tuwaombee wale ambao tayari wamepoteza wapendwa wao kwa mripuko wa coronavirus. Tuombe wapewe nguvu na moyo mkuu wale wanaopitia uzoefu huo wamshikilie Mungu..

SIKU YA 18 - Aprili 13, 2020

KUTAZAMA MBALI KUPITA KINACHOONEKANA

Yesu akamwambia, Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki. (Yohana 20:29)

“Kila mara maisha ya Kikristo yamezingirwa na hatari, na jukumu huonekana kama gumu kulitekeleza. Mawazo yanaona mbele uharibifu unaokaribia, na nyuma utumwa na mauti. Bado sauti ya Mungu inaongea kwa wazi, Nenda mbele. Hebu tuitii amri, hata kama macho yetu hayawezi kupenya giza. Vikwazo vinavyozuia maendeleo yetu kamwe havitatoweka mbele ya roho ya kusitisha, na ya mashaka. Wale wanaoahirisha utii hadi kila mashaka yatoweke, na kusiwe na hatari ya kushindwa, kamwe hawatatii. Imani hutazama mbali zaidi ya magumu, na humshikilia asiyeonekana, yaani Mwenye nguvu zote, kwa hiyo haiwezi kuzuiwa. Imani ni kuushika mkono wa Kristo katika kila dharura. (GW, 262)

Maswali ya Moyoni: Ni rahisi kuamini kile tunachokiona, lakini vipi kuhusu kitu ambacho hatuwezi kukiona? Ni kwa njia gani tunaweza kukuza imani kwa Neno la Mungu ingawa hatujaona utimilifu wake? Kwa kuzingatia Waefeso 2:8 na Matendo 3:16 tunapata wapi hii karama ya ajabu?

Taarifa ya Kusifu: Kwa sababu ya zuio la kusafiri lililosababishwa na COVID-19, kule Papua New Guinea wainjilisi wa hadhara, wachungaji, na wahubiri walei hawawezi tena kusafiri katika nchi hiyo, kwa ajili ya tukio la TMI lililokuwa limepangwa kufanyika mwezi ujao wa Mei. Hata hivyo, watu wa Papua New Guinea tayari walikuwa wanaendelea kuungana pamoja tangu mwaka uliopita, wakiendesha makumi elfu ya Masomo ya Biblia, na kuanzisha maelfu ya mikutano mahalia ikiendeshwa na walei na wachungaji,. Na sasa tayari wanapanga mipango kwa ajili ya msukumo mwingine wa kiinjili utakaofuata baada ya janga la COVID-19 kupita. Hapa tena, lile ambalo adui alitaka liwe kwa ubaya, Mungu analigeuza liwe kwa ajili ya wema mkuu.

MAMBO YA KUOMBEA

1. Omba kwa ajili ya ulinzi wa Mungu kwa watu na nchi ya Papua New Guinea. Mungu aiongoze serikali ya PNG katika kufanya uamuzi, awaongoze wataalamu wake wa afya wanapopambana na COPVID-19
2. Omba kwamba kile anachokifanya Mungu kule PNG kupitia washiriki wa kanisa mahalia kiwe na mafanikio zaidi ya mipango iliyofanywa awali. Kwa vile mipango imewekwa kwa ajili ya kusonga mbele, omba kwamba kusiwe na mapigano ya kikabila.
3. Omba kwa ajili ya waumini ambao wamefungwa katika magereza mbali mbali ulimwenguni. Ombea wawe na ujasiri wa kuwashuhudia wafungwa wenzao wakati wa hii zahama,
4. Ombea kiwanda kidogo cha mikate na kituo cha utume kule Jonkoping, nchini Sweden viweze kuwafikia watu wengi zaidi, ili wengi wamwone Yesu na kumkubali kama Mwokozi wao. Ombea mawasiliano na mazungumzo kwa ajili ya kujifunza Biblia.
5. Ombea makanisa mhalia nchini Sweden, ambayo ni madogo na yenye washiriki wazee. Mungu alete vijana zaidi katika makanisa katika nchi za Skandinavia, na ayalinde haya makusanyiko madogo wakati wa janga hili la COVID-19.

SIKU YA 19 - Aprili 14, 2020

MTAZAME YESU JUU!

“Bwana, asubuhi utaisikia sauti yangu, Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia” (Zab. 5:3)

“Itisha nguvu zako zote kutazama juu, sio chini kwenye magumu yako; ndipo hutazimia njiani. Punde unamwona Yesu nyuma ya wingu, akinyoosha mkono wake kukusaidia; unachotakiwa kufanya ni kumpa tu mkono wako kwa imani rahisi na kumwacha akuongoze. Kwa njia ya imani katika Yesu, unapozidi kuwa mwaminifu, utakuwa na matumaini. Nuru inayong’aa kutoka msalabani Kalvari itakufunulia makadirio ya Mungu juu ya nafsi, na unapoyathamini makadirio hayo, utatafuta kuakisi ile nuru kwa ulimwengu. Jina kubwa miongoni mwa wanadamu ni kama herufi zilizoandikwa juu ya mchanga, bali tabia isiyo na doa itadumu hadi umilele wote. (5 T 578)

Maswali ya Moyoni: Ni jambo gani unalolifanya kila asubuhi? Unatazama habari, barua pepe au mitandao ya kijamii? Je! Unaanza kufikiri juu ya matatizo yako yote? Au unamtazama Yesu juu? Unapoendelea na siku ya leo, jitoe upya kumtazama Yesu badala ya kutazama chini kwenye majaribu yako. Mtazame Yesu kwa ajili ya tumaini badala ya kuugeukia ulimwengu ili kutiwa moyo.

Taarifa ya Kusifu: Katika kipindi cha siku 30 zilizopita, zaidi ya masomo laki moja yalipakuliwa kutoka www.revivalandreformation.org. Tunamshukuru Mungu kwamba watu wengi wanatambua hitaji lao la kiroho na kutafuta kukua katika mwendo wao pamoja na Mungu. Pia tunamsifu Mungu kwamba maelfu ya vikundi vya maombi vinaanzishwa duniani kote kama matokeo ya hili janga la COVID-19.

MAMBO YA KUOMBEA

1. Ombea washiriki wa kanisa katika nchi za Ujerumani, Ufaransa, Hispania, Italia na Ubelgiji. Maeneo haya bado wanapambana kuzuia coronavirus. Ombea uponyaji kwa wale wanaopitia uzoefu wa kupoteza wapendwa wao.
2. Ombea washiriki wa kanisa kule Mashariki ya Kati, na hasa Irani na Israeli. Ombea wale wanaioshi kwenye vyumba vidogo vyenye hewa kidogo na hawana uwezo wa kufanya hata mazoezi.
3. Ombea majirani ambao yawezekana hawamfahamu Yesu. Ombea njia za kushiriki pamoja nao tumaini la Yesu, labda kwa njia ya simu na njia zingine za mtandao.
4. Ombea wale walio katika kanisa lako au jamii yako wanaopambana na COVID-19 sasa hivi. Ombea mkono wa Mungu wa uponyaji uwe pamoja nao.
5. Ombea ili wote tuwe mawakili waaminifu kurudisha zaka na sadaka zetu. Hata kama hali ni ngumu, Biblia inatwambia kwamba wale wanaomheshimu Mungu, naye atawaheshimu (1 Sam.2:30)

SIKU YA 20 - Aprili 15, 2020

MUNGU NI MWAMINIFU!

“Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili” (1 Kor. 10:13)

“Adui hathubutu kwenda umbali wa upana wa unywele mmoja kutoka kwenye eneo lake alilopangiwa. Hakuna nguvu katika jeshi lote la kishetani inayoweza kuilemaza nafsi inayotumainia, kwa ujasiri sahili, hekima inayotoka kwa Mungu. Kristo ni mnara wetu wa uwezo, na Shetani hawezi kuwa na nguvu dhidi ya nafsi inayotembea na Mungu katika unyenyekevu wa moyo. Ahadi kwamba, “Au azishike nguvu zangu, Afanye amani nami; Naam, afanye amani nami” (Isaya 27:5) Katika Kristo kuna msaada mkamilifu na timilifu kwa kila nafsi inayojaribiwa. Hatari zinazingira kila njia, lakini ulimwengu wote wa mbinguni umesimama katika lindo, ili ye yote asijaribiwe zaidi ya lile awezalo kuhimili. (*My Life Today,* uk. 316)

Maswali ya Moyoni: Je! Unahisi kwamba unashughulika na mambo ambayo huwezi kustahimili? Mungu ameahidi kwamba hatatupatia zaidi ya tunayoweza kustahimili, kwa hiyo kama unahisi kuwa umezidiwa dai ahadi ya 1 Kor. 10:13. Dai ahadi ya Wafilipi 4:13, na Zaburi 61:2. Jifariji mwenyewe leo kwa ahadi za Neno la Mungu.

Taarifa ya Sifa: Katika Ulaya yote (na huenda sehemu nyingi kuzunguka ulimwengu), vijana wengi waliokuwa hawaendi kanisani wanajitokeza kwenye vikundi vya kujifunza Biblia mtandaoni. Tunamshukuru Mungu kwa ongezeko hili la shauku kwa Mungu na Neno lake.

1. Omba kwamba vijana wengi zaidi wawe na shauku ya kujifunza Biblia zao. Ombea uamsho mkubwa miongoni mwa vijana.
2. Ombea vijana wetu kote ulimwenguni, wanaoshiriki katika Maombi yao ya Siku 100 yanayoongozwa na idara za Huduma za Vijana na Huduma za Watoto za Konferensi Kuu. Omba kwamba vijana wetu wajifunze kwamba tunapoomba Mungu husikia na kujibu maombi.
3. Ombea walimu wanapopambana kufundisha madarasa kwa nia ya mtandao. Omba Mungu awapatie hekima ya kutumia teknolojia kwa njia yenye manufaa kwa wote. Omba hekima na uvumilivu.
4. Ombea wale waliovunjika mioyo, wale waliopoteza wapendwa wao hivi karibuni, na kwa wale wanaopambana na kutengwa wahisi uwepo wa Mungu
5. Ombea uvumilivu wa madaktari, wauguzi, na wataalamu wa afya walio mstari wa mbele wakipambana na janga la COVID-19.

SIKU YA 21 - Aprili 16, 2020

HEBU TUONGEE IMANI

Sasa najua kuwa Bwana amwokoa masihi wake;Atamjibu kutoka mbingu zake takatifu. Hawa wanataja magari na hawa farasi, Bali sisi tutalitaja jina la Bwana, Mungu wetu. (Zaburi 20:6, 7)

"Lichukue Neno la Mungu kama uhakikisho wako. Je! Hajakualika kwenda kwake? Kamwe usijiruhusu mwenyewe kuongea kwa namna isiyo na tumaini na kukata tamaa. Ukifanya hivyo utapoteza mengi sana. Kwa kuitazama mionekano na kulalamika yanapokuja magumu na shinikizo, unatoa ushahidi wa imani inayoumwa na iliyodhaifu. Zungumza na tenda kana kwamba imani yako haishindwi. Bwana ni tajiri wa rasilimali; anamiliki ulimwengu. Tazama kuelekea mbinguni kwa imani. Mtazame Yeye mwenye nuru na nguvu na ufanisi," (COL, 146)

Maswali ya Moyoni: Kuzungumza na kutenda kwa imani inamaanisha nini? Ikiwa imani yako ni dhaifu, tunakuzaje imani imara? (soma 10:17). Mshirikishe mtu fulani uzoefu ambapo Mungu alikuza imani yako, au mwambie mtu fulani kuhusu maombi yaliyojibiwa.

Taarifa ya Sifa: Tunamshukuru Mungu kwa ujumbe wa afya aliotupatia, unaotuwezesha kuwa imara kupambana na homa na magonjwa. Tunamshukuru Mungu kwa namna anavyotuwezesha kushiriki ujumbe wa afya pamoja na wengine.

MAMBO YA KUOMBEA

1. Omba kwamba Mungu adumu kutusaidia tuwe watu wa imani imara, kwani tunajua majaribu mengi zaidi magumu yako mbele yetu.

2. Ombea kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya watu wa Mungu ili kazi iweze kumalizika na tuweze kwenda nyumbani.

3. Ombea wachungaji na watawala wapewe hekima wanapotafuta kufariji, kutia moyo, na kuongoza katikati ya machafuko.

4. Omba kwamba sisi kama watu tufanye kadiri tuwezavyo kuishi kwa kanuni za afya tulizofundishwa ili miili yetu iwe na mfumo imara wa kinga.

5. Omba kwamba upendo wa Mungu ujae ndani yetu, utuguse, na kuivunja mioyo yetu upya, ili tusinyamaze, bali tuweze kushiriki pamoja na wale wasio na tumaini.